



Je, familia yangu inaweza kustahiki kupata usaidizi wa kifedha hata kama tunapewa bima ya afya kupitia kwa mwajiri wangu?

Ikiwa unafikiri kwamba wewe au wanafamilia wako wanaweza kustahiki kwa usaidizi wa kifedha, wasiliana na NY State of Health ili kupata usaidizi wa kutuma ombi:

Mtandaoni:
nystateofhealth.ny.gov

Kwa simu:
1-855-355-5777 au TTY:
1-800-662-1220

Ana kwa ana:
Usaidizi wa bila malipo kutoka kwa msaidizi aliyeidhinishwa

NY State of Health inafuata sheria za haki za raia za Taifa na sheria za jimbo zinazotumika, na haibagui kwa msingi wa mbari, rangi, jinsia, umri, asili ya kitaifa, imani/dini, hali ya ndoa/familia, rekodi ya kukamatwa, hatia ya(z) jinai, utambulisho wa jinsia, mwelekeo wa kingono, sifa za kinasaba, hali ya jeshi, hali ya mwathiriwa wa unyanyasaji wa nyumbani, na/au kulipiza kisasi.

Bima ya Afya ya Familia Inakuwa ya Bei Nafuu Zaidi

Kanuni Mpya ya Kustahiki kwa Usaidizi wa Kifedha kupitia NY State of Health

- Kuanzia tarehe 1 Januari, 2023, ustahiki wa usaidizi wa kifedha kwa wanafamilia utategemea uwezo wa kumudu kulipia bima ya familia inayotolewa na mwajiri.
- Mpango wa afya wa familia unachukuliwa kuwa “wa bei nafuu” ikiwa gharama yake ni chini ya asilimia 9.02 ya mapato ya kaya.
- Ikiwa bima ya familia inachukuliwa kutokuwa ya bei nafuu, wanafamilia wanaweza kustahili kwa usaidizi wa kifedha.
- Hili halibadilishi tathmini ya uwezo wa kumudika ya wafanyakazi. Ikiwa mfanyakazi anaweza kupata bima ya bei nafuu ya mtu mmoja (mfanyakazi tu) kupitia kwa mwajiri wake, hatatahili kwa usaidizi wa kifedha kupitia NY State of Health. Hata hivyo, wanafamilia wanaweza kustahiki bado.

Kanuni ya Kustahiki kwa Usaidizi wa Kifedha Kabla ya 2023

- Hadi 2023, bima ya afya inachukuliwa kuwa “ya bei nafuu” kwa kutegemea gharama ya bima ya mtu mmoja (mfanyakazi tu).
- Hadi wakati huo, ikiwa gharama ya bima ya mtu mmoja (mfanyakazi tu) ni chini ya asilimia 9.61 ya mapato ya kaya ya mfanyakazi huyo, inachukuliwa kuwa ya bei nafuu. Wafanyakazi wanaoweza kupata bima ya afya ya bei nafuu kutoka kwa mwajiri wao hawatahili kwa usaidizi wa kifedha wa mpango wa NY State of Health.
- Ikiwa mfanyakazi hastahili kwa usaidizi wa kifedha kupitia NY State of Health kwa kutegemea kanuni hii, wanafamilia wa familia ya mfanyakazi huyo pia hawatahili kwa usaidizi wa kifedha kupitia NY State of Health. Hii inatumika hata wakati ambapo mpango wa afya wa familia unaotolewa na mwajiri unagharimu zaidi ya asilimia 9.61 ya mapato ya kaya.

Unaweza Kufanya Nini?

- Tumia Zana ya Kukokotoa Usaidizi wa Kifedha ya NY State of Health: <https://info.nystateofhealth.ny.gov/estimate-financial-assistance>
- Zana hii hutoa ukadiriaji ili kuona ikiwa wewe au wanafamilia wako wanatahili kwa usaidizi wa kifedha. Ustahiki wako halisi utabainishwa ukituma ombi.